# OFISI YA RAISI - TAMISEMI

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI**

**SHULE YA SEKONDARI PEMBA MNAZI**

**S.L.P 36178 DAR ES SALAAM**

Kumb. **Na …………………………** Tarehe **………………..……………..**

Jina la Mwanafunzi **……………………………………………………………………………………**

S.L.P**……………………………………………………………………………………………………**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI PEMBA MNAZI**

**1. UTANGULIZI**

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza (Form one) katika shule hii ya Sekondari Pemba Mnazi kwa mwaka wa masomo **2025.** Shule ya sekondari Pemba Mnazi ipo wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es salaam umbali wa Km 55 kutoka katika kivuko cha kigamboni (Ferry). Usafiri wa basi kutoka Kigamboni unapatikana katika kituo cha mabasi cha Ferry Kigamboni na nauli ya mwanafunzi ni **Tsh.500/=** na unashuka kituo kiitwacho **Chaurembo** kisha utatembea au kupanda pikipiki umbali wa 2.5km

Mhula wa kuanza masomo utaanza tarehe **05/01/2025**, Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **02/01/2025.**

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 Sare za shule**

**a.** Sare ya shule hii ni **mashati meupe 2 ya mikono mifupi**, **suruali mbili (2) Rangi ya Jani la mgomba lililopauka** kwa wavulana na **Sketi mbili (2) Rangi ya jani la mgomba lililopauka kwa wasichana, tai 2 za kijani kwa wavulana, soksi pea 2 Nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana, Mkanda mweusi na T-shirt 1 rangi ya dark blue.** Maelezo ya mshono ni **Linda box kwa sketi za wasichana. Modo na vimini haviruhusiwi**

b. Rangi ya Hijab ni nyeupe isiyo na urembo

c. Sare ya michezo kwa shule yetu ni **bukta na jezi mbili** kwa wavulana wa hostel.

d. Trak-suti nyeusi zilizopita michilizi mitatu meupe .

2.2 Mwanafunzi aje na daftari 11 za couter book Quire 3, kalamu, mkebe wa hesabu na begi.

2.3 Chakula cha mwanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu ni jukumu la mzazi.

2.4 Nauli ya wanafunzi wa bweni kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo, godoro na vifaa vya malazi na matibabu ni jukumu la mzazi

2.5 Mahitaji mengine ya kibinadamu kama mkanda mweusi wa ngozi, viatu vyeusi vinavyofunika miguu visigino vifupi vyenye kamba.

**3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote

inayotolewa na wizara ya Elimlimu chini ya Ofisi ya Raisi –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare ya shule na kuchomekea wakati wote unapotakiwa, uwapo shuleni au unapotoka na kurudi shuleni wakati wote.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na.
i. Kutunza mali za uma

**3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:**

i. Wizi
ii. Uasherati ubakaji na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Uvutaji bangi
v. Makosa ya jinai
vi. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
vii. Kupigana au kupiga
viii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
ix. Kudharau bendera ya Taifa
x. Kupata mimba/kumpa mimba mwanafunzi wa kike ndani na nje ya shule
xi. Kuoa au kuolewa
xii. Kutoa mimba
xiii. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
xiv. Kukataa adhabu kwa makusudi
xv. Kutofika shule kwa siku 90 mfululizo bila taarifa
xvi. Kutofanya mitihani ya shule/Taifa
xvii. Kutoroka shuleni au kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa

**4. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti .shuleni
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI

# SHULE YA SEKONDARI PEMBA MNAZI

**S.L.P 36178 DAR ES SALAAM**

**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI**

PICHA YA MWANAFUNZI

**A. IJAZWE NA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi ………………………………………….
2. Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………….
3. Taifa ……………………………………………………………….
4. Uraia ……………………………………………………………….
5. Dini……………………………………………………………….
6. Shule aliyo/alizo soma kabla ya kuja shuleya Sekondari Pemba Mnazi

| Shule ya Sekondari/Msingi | Tarehe na Mwaka ulionza | Tarehe na Mwaka uliotoka |
|---|---|---|
| i. ……………………… | …………………………… | …………………………… |
| ii. ……………………… | …………………………… | …………………………… |
| iii. ……………………… | …………………………… | …………………………… |
| iv. ……………………….  | …………………………… | …………………………… |

Saini ya mwanafunzi…………………………….. Tarehe……………………………….

PICHA YA MZAZI/MLEZI

**B. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI**

1. Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………………..
2. Utaifa ………………………………………………………….
3. Uraia …………………………………………………………..
4. Anuani ya DSM ……………………………………………...
5. Sehemu anayoishi……………………………………………….
6. Mtaa………………………… Kata……………………………..
7. Namba ya nyumba…………………………………………….
8. Simu: nyumbani……………………… Ofisini……………………………….
9. Mtendaji/Mwenyekiti wa mtaa: Jina……………………………Sahihi…………………… Simu……………………
10. Eleza kama mototo ana matatizo yoyote ya kiafya
…………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………

**C. MAELEZO YA KIKAZI**

i. Jina la mwajiri ………………………………………………………………………...
ii. Anuani ……………………………………………………………………………...
iii. Kazi ya Mzazi/Mlezi ……………………………………………………….........

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi…………………………………………………………………………….……. (majina matatu)

Ambaye ni mzazi/mlezi wa ……………………………………………………………………

Ninaahidi

i. Kumpatia mwanangu mahitaji yake yote muhimu ya shule kama yalivyotajwa katika maelezo ya kujiunga shule kipindi chote cha masomo yake
ii. Kusimamia na kufuatilia mahudhurio yake shuleni na kutoa msaada unaohitajika (maoni, adhabu n.k) katika kumlea mwanangu
iii. Kumpatia matibabu kwa haraka pindi anapougua au kupata changamoto yoyote ya kiafya.
iv. Kulipa fidia juu ya uharibifu/upotevu wa mali ya shule utakaofanywa na mwanangu haraka pindi nipatapo taarifa ya jambo hilo.
v. Kuitikia wito wowote wa kufika shuleni, iwe nimetumiwa ujumbe kwa barua, simu au nimeletewa taarifa ya mdomo na mwanangu kutoka shuleni.
vi. Kusimamia na kufuatilia maendeleo yake kitaaluma na tabia kwa jumla
vii. Kuhakikisha kuwa anajisomea wakati wote awapo nyumbani na kufanya mazoezi yote (Home Works) aliyopewa na walimu kufanyia nyumbani.
viii. Sheria na hatua zichukuliwe dhidi yangu endapo nitashindwa kutimiza ahadi nilizoahidi hapo juu.

Jina…………………………………………………………….…… Saini…………….…………………

Tarehe……………………………………… Simu……………………………………………………

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION (FOMU YA DAKTARI KUTHIBITISHA AFYA YA MWANAFUNZI)**

To be filled by the Government Medical Officer and return to the Head of Pemba Mnazi Secondary School P.O.Box **36178,** Dar es Salaam

TO:
MEDICAL OFFICER:
………………………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………………………..

**PART A:**
**RE:……………………………………………………………………………………………………**
**Please Examine the above named as to his/her fitness for admission as a student in the following common diseases /problems:**

**Put a tick (√) for positive and (X) for negative against in a box provided.**

| NO. | DISEASES / PROBLEMS | (√) | (X) |
|---|---|---|---|
| 1 | Pregnancy | | |
| 2 | Asthma | | |
| 3 | Sight | | |
| 4 | Diabetes | | |
| 5 | Worms (Stool) | | |
| 6 | Epilepsy | | |
| 7 | Tuberculosis (TB) | | |
| 8 | Sickle Cell | | |
| 9 | Heart Disease | | |
| 10 | Yellow Fever | | |
| 11 | U.T.I | | |
| 12 | Malaria | | |
| 13 | Hearing | | |
| 14 | Speech | | |

**Any other ……………………………………………………………………………………………………**

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

**(To be completed by a medical officer)**

**I have examined the above named and consider that he/she is physically Fit / Unfit for admission as above ………………………………………………………………………………………**

**PART C: ANY OTHER ADVICE**

**……………………………………………………………………………………………………………**

**Name…………………………………………………Signature……………………………………..**

**Station……………………………………………… Designation: …………………………………………**

## HUDUMA YA HOSTEL

Shule ina hostel nzuri kwa ajili ya wanafunzi wa kiume tu. Mzazi /Mlezi ambaye mwanae atapangwa kukaa hostel atafuata taratibu zifuatazo:-

**SARE ZA HOSTEL**

- Aje na Suruali mbili (2) nyeusi na Tshirt mbili (2)( za blue bahari zenye nembo ya shule.
- Traki-suti nyeusi zenye michilizi meupe mitatu kwa ajili ya kuvaa usiku hasa kipindi cha baridi kali.
- **Vifaa vingine:** Ndala, ndoo ndogo 1, Taulo, Bukta 1 na Tshirt 1 kwa ajili ya michezo, pasi ya mkaa, sanduku la chuma , mashuka mawili ya light blue, net ya mbu light blue, tochi, nguo za ndani za kutosha na godoro futi 3 Inchi kuanzia 4 na kuendelea.
- Vyombo vya chakula: Wanafunzi wote wa hostel wanatakiwa kuja na sahani, kijiko, bakuli dogo na kikombe.

**AGIZO**

1. Kila mwanafunzi ni lazima aje na ndoo yake pamoja na vyombo vya chakula.
2. Nguo za nyumbani haziruhusiwi shuleni, mwanafunzi atavaa sare za hostel tuu kwa siku zote awapo shuleni baada ya masomo. Nguo za nyumbani zikibainika zitachomwa moto.

## SHERIA ZA HOSTEL

1. **Chakula**
   - Utakula chakula kinachopikwa ndani ya shule tu.
   - Usipeleke, usitunze, usipike au kuchemsha chakula ndani ya bweni au katika eneo la shule.
   - Marufuku kukaa eneo la jiko kama sio muda wa chakula
   - Ni marufuku mwanafunzi kuja na chakula chochote pindi atokapo nyumbani na mzazi haruhusiwi kumletea chakula mwanafunzi pindi anapomtembelea mwanafunzi.

2. **Sare za hostel**
   - Utavaa sare za hostel kila siku baada ya muda wa masomo na siku za mapumziko
   - Nguo nyingine haziruhusiwi. Zikibainika utanyang'anywa na zitachomwa moto.

3. **Usafi na afya**
   - Utapaswa kuwa msafi wa mwili na mavazi kila siku
   - Utafanya usafi ndani na nje ya bweni kila siku.
   - Utapaswa kutibiwa zahanati unapougua na kutumia dawa kwa kuzingatia maelekezo ya daktari. Suala la matibabu ni jukumu la mzazi hivyo mtoto ni lazima aje na bima ya afya.
   - Marufuku kuwa na dawa na kuzitumia bila ya kuwa na maaelekezo ya daktari.

- Dawa za kienyeji na hirizi haviruhusiwi.
- **BIMA YA AFYA NI LAZIMA KWA MWANAFUNZI WA BWENI.**

4. **Mipaka na usalama**
    - Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa. Ukibainika umetoroka utafukuzwa hostel na kuwa mwanafunzi wa kutwa

.

5. **Bwenini**
    - Ni marufuku kumwingiza mgeni yeyote ndani ya bweni.
    - Ni marufuku mwanafunzi kulala nje ya bweni
    - Ni marufuku mwanafunzi kuiba vitu vya wenzake. Ukibainika umeiba utafukuzwa shule
    - Ni marufuku mwanafunzi kupiga/kupigana bwenini. Ukibainika utafukuzwa shule.
    - Ni marufuku kumnyanyasa mwanafunzi mwenzako au kumnyang'anya kitu chochote
    - Ni marufuku kuzurula au kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wote uwapo shuleni. Ukibainika utafukuzwa shule.
    - Ni marufuku kwenda nyumba za walimu bila ruhusa.
    - Mwanafunzi anapaswa kufuata ratiba na utaratibu wa shule muda wote awapo shuleni.
    - Ni marufuku kuwa na zaidi ya Tsh.2000/= bwenini. Pesa zinazozidi kabidhi kwa mwalimu wa bweni au mwalimu wa darasa.
    - Mwanafunzi anapaswa kufika shuleni kabla ya saa 10 jioni siku ya kuripoti au anaporudi kutoka nyumbani.

6. **Uhusiano na wengine**
    - Utawatii walimu, walinzi wa shule, Patron, viranja, viongozi wa bweni na wote wanaokuzidi umri kwa kila agizo jema.
    - Lugha ya matusi, vitisho, wizi au udokozi, ugomvi wa kidini, kupiga na kupigana **ni makosa ya kufukuzwa shule.**
7. **Usalama bwenini**
    - Huruhusiwi kuwa na mishumaa, kemikali au sumu, vitu vyenye ncha kali,na vitu vyenye kulipuka.
    - Usijichubue (Mkorogo), kuwa na vipodozi, mapambo ya mwili (mkufu, herein, pete na bangili), kufanya hivyo ni kosa la kufukuzwa shule.
    - Huruhusiwi kuwa na **simu za mkononi**. Simu ikibainika utanyang'anywa na haitarudishwa.

8. **Ruhusa**
    - Ruhusa kwenda nje ya shule itatolewa kwa sababu maalum na Makamu Mkuu wa Shule. Mwanafunzi anayeruhusiwa lazima aje kuchukuliwa na mzazi/mlezi wake.
    - Hairuhusiwi mzazi/mlezi au ndugu na jamaa kumtembelea mwanafunzi mara kwa mara bila sababu ya msingi na ya lazima.
    - Mzazi/mlezi anaruhusiwa kumtembelea mwanafunzi siku ya **IJUMAA** ya kila **mwisho wa mwezi tu!**
9. **Taaluma**
    - Utoro wa vipindi vya darasani na vya muda wa ziada jioni vitamfanya mwanafunzi husika kuondolewa hostel.
    - Mwanafunzi mwenye wastani chini ya **hamsini (50)** kwenye masomo yake yote ataondolewa hostel.

Ni imani yangu kuwa utazingatia na kutekeleza maagizo yote kikamilifu.
Nakutakia masomo mema na afya njema na Mwenyezi Mungu akutangulie

……………………………..

**NYANDWI M. KAGIZE**
**0712272950**
**MKUU WA SHULE**
**KWA MAELEKEZO PIA PIGA: 0713620945**

**MAKAMU MKUU WA SHLE**

# OFISI YA RAISI - TAMISEMI

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI

## SHULE YA SEKONDARI PEMBA MNAZI

**S.L.P 36178 DAR ES SALAAM**

### KANUNI NA TARATIBU ZA WANAFUNZI WA HOSTEL/BWENI KITAALUMA

Uongozi wa shule kwa kushirikiana na ofisi ya taaluma umeweka utaratibu ufuatao ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa hostel.

**(Ajaze mzazi/mlezi)**

Jina……………………………………… namba ya simu…………………………Uhusiano na mototo ……………………………………….……Anapoishi……………………………………………………….…………
Kazi ya mzazi/mlezi……………………………………………………………………………………………
Sahihi……………………………… tarehe……………………………………

**(Ajaze mwanafunzi mwenyewe)**

Mimi ………………………………………………………………… Kidato cha ………… mwaka ……………

Naahidi nitasoma kwa bidii na kufaulu kwa alama ya wastani wa kuanzia **50%** kwa mitihani ya ndani na nje/Taifa na nitafuata sheria za hostel/bweni . Endapo nitashindwa kufikisha wastani na kufuata sheria za shule nitakuwa tayari kwa hatua zifuatazo :-

1. Kuondolewa hostel
2. Kuwa mwanafunzi wa kutwa (day)
3. Kupangiwa darasa kulingana na alama zangu.

**N.B**

Kama umesoma na kuzikubali taratibu na kanuni hizi jaza sehemu zifuatazo)

Jina……………………………………………………Tarehe…………………Sahihi…………………………

### KWA MATUMIZI YA OFISI TU

**Mkuu washule ……………………….........…………Tarehe……………………Sahihi……………**

**Ofisi ya Taaluma…………………………………….…Tarehe ………………….… Sahihi ……...……**